

# KISWAHILI KIDATO CHA TATU

102/3

KISWAHILI

Karatasi ya 3

FASIHI

MUDA: SAA 2 ½

## MAAGIZO

- a) Jibu maswali manne pekee
- b) Swali la kwanza ni la lazima
- c) Maswali megine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki
- d) Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
- e) Mtahiniwa ahakikishe kwamba kurasa zote za maswali zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

## SEHEMU A

### 1. USHAIRI (LAZIMA)

**Soma shairi lifuatalo kisha njibu maswali.**

WAPENDA MTU KWA KITU

Shairi nakuletewa , tafadhali mwana twaa  
Hikwita hunikimbiya, na kunitiya tamaa  
Kumbe mebadiliniya , hata washenzi watwaa  
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Nilidhani u libasi, njema ya mtu kuvaa  
Hawa sina wasiwasi, popote ninapokaa  
Kumbe u mtu rakhisi , atakaye hukutwaa  
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Usinionye miuja, miuja haitafaa  
Kwamba huna nami haja, ukanambia si baa  
Mtu hupenda kimoja, sende nami kwa hadaa

Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Umejifunza wekevu, kutaka kunihadaa  
Na huno wako uovu, ni bure hautafaa  
Mimi ni wana mtuvu , sitendwi hataataa  
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Kunena mengi nataka, lakini sina wasaa  
Na hapa tulipofika, ni kheri hakuambaa  
Maana u mtu nyoka, huna ahadi ua baa  
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.

Tamati sineni sana, muhibu toa tamaa  
Ulotenda nishaona, wala hutanihadaa  
Sasa kheri kuatana, kulla mtu akakaa  
Una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu.  
(A. Nasir, *Malenga wa mvita, uk 163*)

#### Maswali

- a) Kwa kurejelea vina vya shairi, eleza bahari ya shairi hili. (alama 2)
- b) Eleza maana ya `una mahaba tamaa, wapenda mtu kwa kitu` (alama 2)
- c) Je, msemaji analalamika mambo gani katika shairi? Eleza. (alama 3)
- d) Eleza tabia za mhusika anayezungumziwa katika shairi hili. (alama 3)
- e) Taja na ufafanue tamathali mbili za usemi zilizotumika katika shairi hili. (alama 4)
- f) Eleza dhamira ya mtunzi. (alama 2)
- g) Maneno yafuatayo yameendelezwa kishairi. Yaandike kwa njia sanifu. (alama 4)
- Hikwita \_\_\_\_\_
  - Kulla \_\_\_\_\_
  - Miuja \_\_\_\_\_
  - Kuatana \_\_\_\_\_

## SEHEMU B

### RIWAYA :CHOZI LA HERI

#### JIBU SWALI LA 2 AU 3

2.Fafanua maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii

(alama 20)

3. Lakini itakuwaje historical injustice ,nawe ridhaa,hapo ulipo sicho kitovu chako ?

- a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
- b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumika kwenye dondoo hili (alama 4)
- c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya (alama 6)
- d) Ni mambo gani yaliyo wakumba wale ambao kitovu chao sicho walicho (alama 6)

### SEHEMU C: TAMTHILIA KIGOGO

#### JIBU SWALI LA 4 AU 5

4.) Thibitisha anwani ya Tamthilia Kigogo(al 20)

Au

5) Jadili mbinu anazotumia Majoka kuongoza Sagamoyo(al 20)

### SEHEMU D: HADITHI FUPI TUMBO LISILOSHIBA

#### JIBU SWALI LA 6 AU 7

6) Anwani Tumbo lisiloshiba ni faafu. Jadili(al 20)

Au

7) usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto. Rudi,rudi kwa mola wako.

- a) Eleza muktadha wa dondoo hii (al 4)
- b) Fafanua sifa za msemewa (al 6)
- c) Tambua tamathali ya usemi iliyotumika hapo juu (al 4)
- d) Ni kwa nini msemewa anatakikana kurudi kwa mola wake? (al 6)

### SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI

8.

- a. Fafanua maana ya istilahi zifuatazo (al 5)
  - i. Kisasili
  - ii. Lakabu
  - iii. Kitendawili
  - iv. Ushairi simulizi
  - v. Ngomezi
- b.
  - i. Taja vianzio viwili vya ngano (al 2)
  - ii. Eleza majukumu matatu ya vianzio vya ngano (al 3)

- c.
- i. Eleza sifa mbili za mtambaji bora (al 2)
  - ii. Tambulisha nyiso (al 1)
  - iii. Jadili majukumu mawili ya nyiso katika jamii (al 2)
- d.
- i. Eleza maana ya misimu (al 2)
  - ii. Fafanua sifa za misimu (al 3)

for free past papers visit [www.freekcsepastpapers.com](http://www.freekcsepastpapers.com)